**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**BODI YA KAHAWA TANZANIA**

# TANGAZO

## UFAFANUZI KUHUSU TANGAZO LA UFUNGUZI WA MSIMU WA KAHAWA 2025/2026

Bodi ya Kahawa Tanzania ilitoa tangazo kwa umma kuhusu tarehe za kuanza kwa msimu wa kahawa 2025/2026 katika kanda zote za uzalishaji. Tangazo hilo lilitolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 23 (1) ya Kanuni za Kahawa 2013. Bodi inatoa ufafanuzi kwamba, kwa kuwa mwaka huu wa 2025 msimu wa mavuno ya kahawa katika maeneo mengi ya uzalishaji unatarajiwa kuanza mapema zaidi, hivyo muda uliobaki hautoshi kwa wadau wa kahawa kufanya maandalizi ya kutosha ili kutekeleza utaratibu ulioelekezwa na Bodi wa kuanza kufanyika kwa minada ya kahawa ghafi za Arabika laini (Arabica Parchment Coffee Auctions).

Hivyo Bodi inatoa taarifa kuwa, katika msimu wa 2025/2026 utaratibu wa mauzo ya kahawa utaendelea kama ilivyokuwa msimu uliokwisha wa 2024/2025. Masuala mengine yaliyotakiwa kuzingatiwa katika tangazo hilo yanaendelea kubakia kama yalivyofafanuliwa katika Tangazo hilo.

Bodi inawakumbusha wanunuzi wa kahawa, wenye viwanda na wawezeshaji wengine walioingia makubaliano ya kilimo cha mkataba na Vyama vya Ushirika kuwasilisha makubaliano yao kwa ajili ya tathimini na ufuatiliaji kwa mujibu wa Kanuni ya 59.

Primus O. Kimaryo

**<u>MKURUGENZI MKUU</u>**

**BODI YA KAHAWA TANZANIA**

**S. L. P. 732 – Moshi, Simu: 027-2752324**

**Barua pepe: info@coffee.go.tz; Tovuti: www.coffee.go.tz**